*Kanisa la Waadventista Wasabato – Jimbo la Mara*

**SHULE YA SEKONDARI IKIZU**

Tovuti: www.ikizuhighschool.ac.tz

Barua pepe: ikizuhigh@gmail.com

S.L.P. 245, MUSOMA-TANZANIA

MKUU WA SHULE +255 752 999 350

MAKAMU WA SHULE +255 784 344 013

MHAZINI WA SHULE +255 621 074 521

Mwl. TAALUMA +255 693 425 060

Mpendwa, ______________________________________________

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA IKIZU KIDATO CHA KWANZA 2024.**

Napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kuingia kidato cha KWANZA hapa Ikizu mwaka 2024. Shule hii inamilikiwa na kuendeshwa na Kanisa la Waadventista Wasabato na inatoa elimu ya kidato cha kwanza hadi cha sita kwa wavulana na wasichana. Tunaamini kuwa huu ni mpango wa Mungu kwako kupata nafasi hii adimu ya masomo ya Sekondari hapa Ikizu. Unaombwa kuitumia kwa busara, sala, bidii na nidhamu ili gharama kubwa za kukusomesha zilete manufaa makubwa kwako, kwa Ndugu zako na kwa Taifa letu.

## A. MAHALI SHULE ILIPO

Shule ya Sekondari Ikizu ipo mkoa wa Mara, Wilaya ya Bunda, kata ya Nyamuswa kijiji cha Bukama. Shule inafikika kiurahisi kwa usafiri wa magari ya abiria toka Bunda Mjini, Mugumu au Musoma Mjini (stendi ya Bweri). **Mwanafunzi atapokelewa siku ya Jumapili hadi Ijumaa kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 11:00 jioni.**

## B. TAARIFA BINAFSI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI ______________________________
2. TAREHE YA KUZALIWA ______________________________
3. SHULE YA MSINGI ALIYOSOMA ____________________ WILAYA: ______________
4. DHEHEBU ______________________________

## TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. JINA LA MZAZI/MLEZI ______________________________
2. KAZI YAKE ______________________________
3. MAHALI ANAPOISHI
   MTAA/KIJIJI ______________________________
   WILAYA ______________________________
   MKOA ______________________________
4. NAMBA YA SIMU (YENYE WHATSAP KAMA IPO) ______________________________

- **Shule itafunguliwa tarehe 04/01/ 2024.**

## C. SARE NA MAHITAJI YA SHULE KWA MWANAFUNZI.

1. SARE ZA SHULE

**1.1. Wasichana:**

- Sketi mbili **Nyeusi** zenye marinda (kitambaa cha suti), urefu hadi chini
- Shati 2 nyeupe, mikono mifupi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyofunika mguu vyenye kamba visigino vifupi.
- Soksi ndefu nyeupe (stocking) jozi 2 au Zaidi.
- Track Suti ya Blue kwa wasichana kwaajili ya michezo.
- Raba kwaajili ya michezo
- Viatu vya wazi vyeusi (open shoes) pair moja huvaliwa baada ya saa za darasani **(si yeboyebo).**
- Nguo ya kulalia (night dress) nyepesi.
- Sketi ya solo nyeusi kwa ajili ya sare ya kanisani urefu hadi chini
- Shati la light blue lenye mikono mirefu kwaajili ya siku ya Ibada.
- Sketi ya light blue ya solo, urefu usawa wa goti pamoja na T-shirt ya blue/nyeupe aina ya Taifa Stars kwaajili ya michezo.
- Shamba dress (sketi ya marinda, rangi ya ugoro, urefu hadi chini) huvaliwa baada ya saa za darasani.

1.2. Wavulana:

- Suruali 2 **Nyeusi** zenye marinda mawili yenye mifuko 2 (miwili) pembeni, nyuma mfuko (1) mmoja upande wa kulia, Size Inchi 16 mzunguko wa chini.
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Shati 2 nyeupe mikono mifupi
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika miguu vyenye kamba na visigino vifupi (sio buti)
- Soksi nyeusi jozi mbili (2) au Zaidi.
- Track suti ya kijani (Green) kwaajili ya michezo
- Viatu vya wazi vyeusi (open shoes) pair moja. Huvaliwa baada ya saa za madarasa (**siyo yeboyebo**).
- Suti nyeusi kwa ajili ya uniform ya kanisani, koti la kola, lenye mikono mirefu lenye vishikizo viwili.
- Shati la light blue lenye mikono mirefu kuvalia suti siku ya ibada (Jumamosi) tu.
- Fulana za kuvalia ndani 2 au zaidi nyeupe.
- Raba za michezo, bukta na Tshirt za michezo blue/nyeupe aina ya Taifa Stars.
- Suruali ya ugoro ambayo huvaliwa baada ya saa za darani.

Tafadhali njoo na vifaa vifuatavyo au waweza kuvipata shuleni kwa bei zilizoainishwa hapo chini:-

*2.* MAHITAJI YA BWENINI

| | |
|---|---|
| Kikombe | 500/= |
| Sahani | 2,000/= |
| Kijiko | 500/= |
| Tochi 1 | 2,000/= |
| Chandarua | 10,000/= |
| Toilet papers 6 kila muhula(1@500/=) | 3,000/= |
| Galoni ya maji ya kunywa lita 5 | 2,000/= |
| Ndoo ya plastiki 1 lita 10 au 20 | 3,500/= |
| Kandambili | 3,000/= |

*3.* KWA AJILI YA MASOMO AJE NA VITU HIVI.

| | |
|---|---|
| Mathematical set. | 3,500/= |
| Faili 1 (Spring file) | 3,000/= |
| Graph pad 02 | @ 3,000/= |
| Penseli na kifutio | @ 100/= |
| Rula 1 | 500/= |
| Kalamu za wino 5 au Zaidi | @ 200/= |

- **Kamusi ya Kiingereza (Oxford Learners dictionary) ni lazima**
- **Sanduku la mbao au chuma lenye kufuli 1(Sanduku lisiwe la bati)**
- **Vitabu vya TAI kwa masomo ya Civics, Kiswahili, English, History, Geography, Basic Mathematics, Biology, Physics, Chemistry, Agriculture na au Computer studies ni vya muhimu. Isipokuwa vya Basic Mathematics na English Language ni vya lazima.**

MUHIMU

- **Mwanafunzi atapewa godoro, blanketi, shuka(2), madaftari (Counter book 12), sweta 1, T-shirt 2, Tai kwa mvulana Skafu kwa msichana, Kitabu cha nyimbo, Biblia ya Kiingereza, Kitabu cha sheria za shule (student's handbook), Lesson pamoja na kitambulisho bila malipo yoyote anapowasili shuleni.**
- Njoo na Picha (Passport size) za watu watatu watakao kuwa wanakutembelea hapa shuleni.
- **NGUO ZA NYUMBANI NI MARUFUKU** kwa wasichana na Wavulana.

D. MAMBO YA KIROHO

Shule hii hutoa elimu ya kiroho sambamba na elimu dunia. Unapowasili tafadhali kwa kicho na unyenyekevu mtafute Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na roho yako yote na kwa akili zako zote. Suala la Ibada ni la lazima kwa wanafunzi wote ikiwemo utunzaji wa SABATO.

Shule hii inakukaribisha kujiunga na kwaya, chama cha vijana (**AY, AMBASADOR na PFC**) na program zote za kiroho. Usifiche wala kuogopa kutumia vipaji mbalimbali ambavyo Mungu amekujalia. Kwa watakaopenda kujiunga na vyama vya vijana waje na sare/uniform ya chama husika.

KARIBU SHULE YA SEKONDARI IKIZU

…………………………
BOREGA P. BOREGA
MKUU WA SHULE

IKIZU SECONDARY SCHOOL HEAD OF SCHOOL P.O. Box 245 MUSOMA

## E. MACHANGANUO WA ADA NA MAHITAJI MENGINE

MCHANGANUO WA ADA KWA MWAKA 2024 (O-LEVEL)

| | KIDATO | JANUARI | APRILI | JULAI | SEPTEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| BWENI | I | 700,000 | 350,000 | 700,000 | 350,000 | 2,100,000 |
| | II | 700,000 | 350,000 | 700,000 | 350,000 | 2,100,000 |
| | III | 700,000 | 350,000 | 700,000 | 350,000 | 2,100,000 |
| | IV | 700,000 | 350,000 | 700,000 | 350,000 | 2,100,000 |
| KUTWA | I | 600,000 | 250,000 | 600,000 | 250,000 | 1,700,000 |
| | II | 600,000 | 250,000 | 600,000 | 250,000 | 1,700,000 |
| | III | 600,000 | 250,000 | 600,000 | 250,000 | 1,700,000 |
| | IV | 600,000 | 250,000 | 600,000 | 250,000 | 1,700,000 |

- Malipo yote yafanyike Benki kwenye akaunti namba zifuatazo:

| | |
|---|---|
| NMB Bank A/C | 30302300966 |
| NBC Bank A/C | 030103000830 |

Jina la akaunti ni IKIZU HIGH SCHOOL

Andika jina la mwanafunzi na kidato kwenye bank slip siyo jina la aliyelipa.

NB:

- Njoo na Rimu A4 Double A kama ilivyoainishwa hapa chini
  Januari – Rimu I
  Julai -- Rimu I
- Kama mwanao anayo BIMA YA AFYA (NHIF) Aje nayo, ambao hawana watatakiwa kulipia gharama hizo ambazo ni Tsh 50,400/= na shule itashughulikia kupata Bima hiyo.
- Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mwanafunzi/mtoto ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/ MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA KUWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO :-

MAKAMU WA SHULE +255 784 344 013

+255 759 346 439

MHAZINI WA SHULE +255 621 074 521

Mwl. TAALUMA +255 693 425 060

MWANDAMIZI MALEZI (MATRONI) +255 756 663 663

MWANDAMIZI MALEZI (PATRONI) +255 752 811 691

## MKATABA WA KUMSOMESHA MWANAFUNZI KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKIZU.

**Huu ni mkataba wa kumsomesha mtoto hapa Ikizu Sekondari unaofanywa kati ya SHULE YA SEKONDARI IKIZU na Ndugu__________________________________ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi_________________________________________ambaye amepata nafasi ya kusoma hapa Ikizu Sekondari katika kidato cha____________________**

### A. MASHARTI YA/SHERIA ZA SHULE

Yafuatayo ni masharti ya shule ambayo mzazi/mlezi inambidi ayaelewe na ayaridhie kabla mtoto hajapokelewa shuleni.

1. Karo na michango yoyote ikishalipwa na mtoto akaamua kuhama au kuacha shule **haitarudishwa.**
2. Karo na michango ikishalipwa haitabadilishwa kutoka kwa mtoto mmoja hadi mwingine.
3. Kupiga au kupigana ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake ni kufukuzwa shule.
4. Kumgomea mwalimu au mfanyakazi au kuhamasisha mgomo wa shule ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
5. Ulevi wa pombe, uvutaji sigara au madawa ya kulevya ni mwiko hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
6. Wizi wowote ama uharibifu wa mali ya shule ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
7. Uasherati na mahusiano ya jinsi moja ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake ni kufukuzwa shule
8. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule ni kosa kubwa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule.
9. Kwenda kwenye miji ya watumishi bila ruhusa ni marufuku.
10. Kukwepa masomo au mitihani na kutohudhuria vipindi bila ruhusa ya mwalimu wa somo au wa zamu ni kosa kubwa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
11. Udanganyifu katika mitihani yoyote hapa shuleni ni marufuku na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
12. Kudharau, kukwepa au kukashifu ibada zinazoendeshwa shuleni ni kosa na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule
13. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, watumishi, walezi na jamii kwa ujumla ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa kufukuzwa shule.
14. Kumiliki simu, radio, camera na vitu vyote vya aina hiyo ni marufuku hapa shuleni na adhabu yake yaweza kuwa ni kufukuzwa shule. Aidha vikikamatwa havitarudishwa kwa mtoto.
15. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua au kuua ni kosa na adhabu yake ni kufukuzwa shule.
16. Wastani wa ufaulu wa wanafunzi mwisho wa mwaka kutoka kidato hadi kidato ni 45%. Mwanafunzi asiyefikia wastani atatakiwa kukariri kidato au kuhamia shule nyingine.
17. Tarehe ya kufika shuleni ni tarehe ya kufungua shule. Kila mwanafunzi afike shuleni siku hiyo bila kukosa vinginevyo hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.
18. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza. Kila mwanafunzi ajitahidi kuongea lugha hiyo ili kukwepa adhabu inayoweza kutolewa kwake akiongea lugha isiyorasmi.
19. Ni marufuku kudharau alama za Taifa letu. Mfano; wimbo wa taifa, Bendera ya Taifa, fedha n.k
20. Ni marufuku mwanafunzi kuja na chakula cha aina yoyote shuleni au mzazi/mlezi kumletea mwanafunzi chakula shuleni.
21. Endapo mzazi/mlezi atahitaji kufatilia maendeleo ya mtoto shuleni basi afike siku za kazi kuanzia saa 2 Asubuhi mpaka saa 9 Alasiri.
22. Somo la Bible knowledge ni la lazima kwa kila mwanafunzi

### B. TAMKO LA MWANAFUNZI

Mimi __________________________________________ Wa kidato cha ____________________

Nimeyasoma masharti ya shule na ninakubaliana nayo.

Sahihi ya Mwanafunzii: __________________ Tarehe:________________

### C. TAMKO LA MZAZI

Mimi __________________________________________

Mzazi/Mlezi wa ____________________________________ Nimeyasoma masharti ya shule na ninakubaliana nayo.

Sahihi ya mzazi/mlezi:__________________Tarehe:________________

**NB: Fomu hii ni lazima ikabidhiwe kwa Makamu Mkuu wa shule kabla ya usajili wa mtoto shuleni.**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**Ref. No IKHS/**

The Medical officer

………………………………

……………………………….

……………………………….

Please examine ………………………………………………as to his/her fitness for pursuing Secondary Education at this School

p

1. Hemoglobin …………………………………………………
2. P.V. Bleeding ……………………………………………….
3. (a) Sight ……………………………………………………..

   (b) Hearing …………………………………………………..
4. Blood pressure …………………………………………………
5. Sickle Cell Test …………………………………………………
6. Deformit …………………………………………………………
7. Urine for sugar & pregnancy test ………………………………….
8. Epileps ………………………………………………………….
9. Leprosy ………………………………………………………….
10. Heart Examination ………………………………………………
11. Tumors – breast ………………………………………………….
12. Pulmonary tuberculosis …………………………………………
13. Stool for routine Examination ……………………………………..
14. Asthma …………………………………………………………
15. Skin diseases ……………………………………………………..

**Comments …**……………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………….

**NAME ………………………………… ……….SIGNATURE …………… DESIGNATION…………………**

**STATION ……………………… ………OFFICIAL STAMP …………………..DATE …………………...**